05


OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua, 2321, MMP, Zanzibar
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136


# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI KWA ZANZIBAR, MEI, MWAKA 2023

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

**Utangulizi**
Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.


Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (12).

**Lengo**
Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

**Ajali za Barabarani**


Jumla ya ajali 12 zimeripotiwa mwezi wa Mei, 2023. Wilaya Kaskazini "B", Micheweni na Mkoani zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni mbili (2) kwa kila wilaya.

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Mei 2023**





Idadi ya Ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Mei , 2023 imepungua kwa asilimia 20.0 kutoka ajali 15 kwa mwezi wa Aprili hadi ajali 12 kwa Mwezi wa Mei 2023.
Kwa mwezi wa Mei 2023, wilaya Kaskazini "B", Micheweni na Mkoani zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni mbili (2) kwa kila wilaya ikilinganishwa na Mwezi wa Aprili ambapo Magharibi 'B' imeripotiwa kuwa na Ajali nyingi (4).

**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwezi wa Aprili 2023 na Mei 2023**




Idadi ya Ajali za barabarani kwa mwaka uliopita imepungua kwa asilimia 25.0 kutoka ajali 16 kwa mwezi wa Mei 2022 hadi ajali 12 kwa mwezi wa Mei 2023. Kwa mwezi wa Mei, 2023, wilaya Kaskazini "B", Micheweni na Mkoani zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni mbili (2) kwa kila wilaya ikilinganishwa na Mwezi wa Mei 2022 ambapo Kaskazini 'B' imeripotiwa kuwa na Ajali nyingi (5).

**Kielelezo 1.3: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani Kwa Mwezi wa Mei 2022 na Mei 2023**





Jumla ya waathirika 28 wameripotiwa mwezi wa Mei, 2023, ambapo waathirika 21 walikuwa wanaume na waathirika saba (7) walikuwa wanawake. Wilaya ya Mkoani imeripotiwa kuwa na waathirika wengi ambao ni 12 sawa na asilimia 42.9 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Mei 2023**





Waathirika waliofariki kwa mwezi Mei imepungua kwa asilimia 50.0 kutoka waathirika waliofariki 12 kwa mwezi wa Aprili 2023 hadi waathirika sita (6) kwa mwezi wa Mei 2023.

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Aprili 2023 na Mei 2023**




Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi uliopita imeongezeka kutoka waathirika 13 kwa mwezi wa Aprili 2023, hadi waathirika 22 mwezi wa Mei, 2023.

**Kielelezo 1.6: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Aprili 2023 na Mei 2023**





Waathirika Waliofariki kwa mwaka uliopita imepungua kwa asilimia 40.0 ambapo kwa mwezi wa Mei 2022 walikuwa waathirika 10 wakati kwa mwezi wa Mei, 2023 walikuwa waathirika sita (6).

**Kielelezo 1.7: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Mei 2022 na Mei 2023**





Waathirika waliojeruhiwa kwa mwaka uliopita imeongezeka ambapo kwa mwezi wa Mei 2022 walikuwa majeruhi 11 wakati kwa mwezi wa Mei, 2023 walikuwa majeruhi 22.

**Kielelezo 1.8: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Mei 2022 na Mei 2023**




Waathirika wengi inaonekana ni Abiria. Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani (waliojeruhiwa na waliofariki), Abiria ni 11, Wapanda baskeli na pikipiki nane (8), Waendao kwa miguu watano (5) na Dereva wanne (4).

**Kielelezo 1.9: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Mei 2023**





Kwa mwezi wa Mei 2023, ajali zaidi zilitokea muda wa saa 9:01jioni - 3:00 usiku ambapo zimeripotiwa ajali sita (6) na 9:01 usiku - 12:00 asubuhi zimeripotiwa ajali tatu(3).

**Kielelezo 1.10: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Mei 2023**




Jumla ya ajali 12 zilizoripotiwa mwezi wa Mei, 2023 kati ya hizo, ajali 8 zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali nne (4) zimesababishwa na uzembe wa madereva. Mkoa wa Kaskazini Pemba unaongoza kuwa na ajali zilizosababishwa na mwendo kasi (ajali 3) na Kusini Pemba unaongoza kua na ajali zilizosababishwa na uzembe wa madereva (ajali 3).

**Kielelezo 1.11: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa Mei 2023**




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 3,620 yameripotiwa mwezi wa Mei, 2023, ambapo makosa 3,614 yamefanywa na wanaume na makosa sita (6) yamefanywa na wanawake. Wilaya ya Kati ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 894 ) sawa na asilimia 24.7 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa. Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ambayo ni makosa 32 (asilimia 0.9).

Wilaya za Mkoa wa Kusini Unguja zimechangia asilimia 32.3 ya makosa yote yaliyoripotiwa, hivyo mkoa huo unaongoza kwa makosa ya barabarani (makosa 1,169) ikifuatia wilaya za mkoa wa Mjini Magharibi (Makosa 1,039) sawa na asilimia 28.7.


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Mei 2023**




Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Mei, 2023 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 940) yakifuatia na Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (makosa 683), Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia (makosa 561) na Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria (makosa 519) .


Orodha ya makosa haya manne (4) ya barabarani kati ya yote tisa (9) yaliyoripotiwa yamechangia asilimia 74.7.

**Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani,Mei 2023**




Idadi ya makosa kwa mwezi uliopita imepungua kwa asilimia 1.6 kutoka makosa 3,680 mwezi wa Aprili 2023 hadi 3,620 mwezi wa Mei 2023.Wilaya ya Kati iliongoza kwa mwezi wa Aprili 2023 (makosa 779) ambapo pia wilaya Kati inaongoza kwa mwezi wa Mei 2023 (makosa 894).

**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Mwezi wa Aprili 2023 na Mei 2023**




Idadi ya makosa kwa mwaka uliopita imeongezeka kwa mwezi wa Mei, 2023 ambapo kwa mwezi wa Mei 2022 yaliripotiwa makosa 1,775 wakati kwa mwezi wa Mei 2023 yameripotiwa makosa 3,620.Wilaya ya Mjini iliongoza zaidi kwa makosa ya barabarani (makosa 262)kwa mwezi wa Mei, 2022 ambapo wilaya Kati inaongoza kwa mwezi wa Mei 2023 (makosa 894).

**Kiel elezo 2.3: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Mwezi wa Mei 2022 na Mei 2023**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (12). Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 12 zimeripotiwa mwezi wa Mei, 2023. Wilaya Kaskazini "B", Micheweni na Mkoani zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni mbili (2) kwa kila wilaya. Mlinganisho wa idadi ya Ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Mei imepungua kwa asilimia 20.0 kutoka ajali 15 kwa mwezi wa Aprili hadi ajali 12 kwa mwezi wa Mei 2023.

Jumla ya makosa 3,620 yameripotiwa mwezi wa Mei, 2023, ambapo makosa 3,614 yamefanywa na wanaume na makosa sita (6) yamefanywa na wanawake. Wilaya ya Kati ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 894 ) sawa na asilimia 24.7 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa. Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Mei, 2023 ni "Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 940)".

**ANNEX:**

**Jadweli 3.0: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Mei 2023**

| Wilaya | Idadi ya ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nambari | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 1 | 8.3 | 1 | 0 | 1 | 16.7 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 3.6 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 16.7 | 0 | 1 | 1 | 16.7 | 1 | 0 | 1 | 4.5 | 1 | 1 | 2 | 7.1 |
| Kati | 1 | 8.3 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 0 | 2 | 9.1 | 2 | 0 | 2 | 7.1 |
| Kusini | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Mjini | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 8.3 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 8.3 | 1 | 0 | 1 | 16.7 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 3.6 |
| Wete | 1 | 8.3 | 1 | 0 | 1 | 16.7 | 2 | 0 | 2 | 9.1 | 3 | 0 | 3 | 10.7 |
| Micheweni | 2 | 16.7 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 4.5 | 1 | 0 | 1 | 3.6 |
| Chake chake | 1 | 8.3 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 3 | 3 | 6 | 27.3 | 3 | 3 | 6 | 21.4 |
| Mkoani | 2 | 16.7 | 2 | 0 | 2 | 33.3 | 7 | 3 | 10 | 45.5 | 9 | 3 | 12 | 42.9 |
| **Zanzibar** | **12** | **100** | **5** | **1** | **6** | **100** | **16** | **6** | **22** | **100** | **21** | **7** | **28** | **100** |

**Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Mei 2023**

| Wilaya | Idadi ya ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda baskeli na pikipiki | | | | | | Waendao kwa miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wa liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Wa liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Wa liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Wa liokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 |
| Kati | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Chake chake | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 2 | 3 | 5 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| **Zanzibar** | **12** | **2** | **0** | **2** | **2** | **0** | **2** | **1** | **0** | **1** | **4** | **6** | **10** | **1** | **0** | **1** | **7** | **0** | **7** | **1** | **1** | **2** | **3** | **0** | **3** |

## Jadweli 3.2: Mlinganisho wa Takwimu za Ajali Barabarani kwa Mwezi wa Mei 2022 na Mei 2023

| Wilaya | Idadi ya ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 | Mei - 22 | Mei - 23 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 2 | 3 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 1 | 0 | 1 |
| Kati | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 0 | 3 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 2 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Micheweni | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Chake chake | 1 | 1 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 2 | 0 | 10 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 5 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **16** | **12** | **11** | **22** | **10** | **6** | **1** | **2** | **1** | **2** | **1** | **10** | **2** | **1** | **4** | **7** | **3** | **1** | **5** | **3** | **4** | **2** |

### Jadweli 3.3: Mlinganisho wa Takwimu za Ajali Barabarani kwa Mwezi Aprili 2023 na Mei 2023

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Walioathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda baskeli na pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 |
| Kaskazini 'A' | 3 | 1 | 4 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Kati | 2 | 1 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 2 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 4 | 1 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 1 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 1 | 1 | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 1 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 2 | 2 | 10 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 5 | 0 | 1 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **15** | **12** | **13** | **22** | **12** | **6** | **0** | **2** | **0** | **2** | **2** | **10** | **1** | **1** | **10** | **7** | **8** | **1** | **1** | **3** | **3** | **2** |

## Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Mei 2023

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji hatari | | | Ubovu wa vipando | | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 30 | 0 | 30 | 208 | 0 | 208 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 10 | 0 | 10 | 2 | 0 | 2 | 72 | 0 | 72 | 93 | 0 | 93 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 31 | 0 | 31 | 391 | 0 | 391 | 13 | 0 | 13 | 217 | 0 | 217 | 117 | 0 | 117 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 15 | 0 | 15 | 51 | 0 | 51 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 | 0 | 26 | 60 | 0 | 60 | 22 | 0 | 22 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 31 | 0 | 31 | 0 | 0 | 0 | 113 | 0 | 113 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 39 | 0 | 39 | 24 | 0 | 24 | 17 | 0 | 17 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 | 0 | 16 | 92 | 0 | 92 | 25 | 0 | 25 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 15 | 0 | 15 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 6 | 26 | 23 | 0 | 23 | 19 | 0 | 19 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 | 0 | 26 | 13 | 0 | 13 | 18 | 0 | 18 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **0** | **34** | **0** | **34** | **405** | **0** | **405** | **185** | **6** | **191** | **561** | **0** | **561** | **683** | **0** | **683** |

## Inaendelea… Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Mei 2023

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 146 | 0 | 146 | 217 | 0 | 217 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 606 | 0 | 606 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 38 | 0 | 38 | 197 | 0 | 197 | 0 | 0 | 0 | 414 | 0 | 414 |
| Kati | 7 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 23 | 0 | 23 | 95 | 0 | 95 | 0 | 0 | 0 | 894 | 0 | 894 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 105 | 0 | 105 | 94 | 0 | 94 | 0 | 0 | 0 | 275 | 0 | 275 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 38 | 0 | 38 | 103 | 0 | 103 | 0 | 0 | 0 | 249 | 0 | 249 |
| Magharibi 'A' | 34 | 0 | 34 | 0 | 0 | 0 | 56 | 0 | 56 | 186 | 0 | 186 | 0 | 0 | 0 | 420 | 0 | 420 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 84 | 0 | 84 | 0 | 0 | 0 | 206 | 0 | 206 | 0 | 0 | 0 | 370 | 0 | 370 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 9 | 28 | 0 | 28 | 0 | 0 | 0 | 170 | 0 | 170 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 | 8 | 1 | 0 | 1 | 6 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 32 | 0 | 32 |
| Chake chake | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 14 | 0 | 14 | 12 | 0 | 12 | 0 | 0 | 0 | 90 | 6 | 96 |
| Mkoani | 6 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 18 | 0 | 18 | 13 | 0 | 13 | 0 | 0 | 0 | 94 | 0 | 94 |
| **Zanzibar** | **49** | **0** | **49** | **238** | **0** | **238** | **519** | **0** | **519** | **940** | **0** | **940** | **0** | **0** | **0** | **3,614** | **6** | **3,620** |

## Jadweli 3.5: Takwimu za Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Mei, 2022 na Mei, 2023

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji hatari | | Ubovu wa vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 4 | 3 | 0 | 32 | 30 | 72 | 208 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 45 | 2 | 0 | 10 | 10 | 2 | 4 | 72 | 50 | 93 |
| Kati | 0 | 0 | 67 | 31 | 17 | 391 | 31 | 13 | 38 | 217 | 71 | 117 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 12 | 10 | 10 | 15 | 6 | 51 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 63 | 26 | 100 | 60 | 36 | 22 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 63 | 31 | 69 | 0 | 16 | 113 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 0 | 68 | 39 | 87 | 24 | 19 | 17 |
| Wete | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 13 | 16 | 38 | 92 | 23 | 25 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 5 | 15 | 15 | 0 |
| Chake chake | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 8 | 26 | 15 | 23 | 13 | 19 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 26 | 32 | 13 | 36 | 18 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **117** | **34** | **55** | **405** | **292** | **191** | **430** | **561** | **357** | **683** |

**Inaendelea… Jadweli 3.5: Takwimu za Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Mei, 2022 na Mei, 2023**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 11 | 146 | 0 | 217 | 58 | 0 | 0 | 0 | 179 | 606 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 38 | 79 | 197 | 0 | 0 | 213 | 414 |
| Kati | 9 | 7 | 0 | 0 | 21 | 23 | 7 | 95 | 0 | 0 | 261 | 894 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 105 | 0 | 94 | 0 | 0 | 39 | 275 |
| Mjini | 0 | 0 | 21 | 0 | 0 | 38 | 32 | 103 | 0 | 0 | 262 | 249 |
| Magharibi 'A' | 0 | 34 | 0 | 0 | 12 | 56 | 32 | 186 | 0 | 0 | 197 | 420 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 84 | 18 | 0 | 20 | 206 | 0 | 0 | 227 | 370 |
| Wete | 1 | 0 | 0 | 0 | 7 | 9 | 72 | 28 | 0 | 0 | 156 | 170 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 8 | 1 | 1 | 23 | 6 | 0 | 0 | 45 | 32 |
| Chake chake | 0 | 2 | 0 | 0 | 12 | 14 | 18 | 12 | 0 | 0 | 68 | 96 |
| Mkoani | 0 | 6 | 0 | 0 | 15 | 18 | 25 | 13 | 0 | 0 | 128 | 94 |
| **Zanzibar** | **10** | **49** | **32** | **238** | **116** | **519** | **366** | **940** | **0** | **0** | **1,775** | **3,620** |

## Jadweli 3.6: Takwimu za Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Aprili 2023 na Mei 2023

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji hatari | | Ubovu wa vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 25 | 1 | 44 | 4 | 1 | 0 | 66 | 30 | 95 | 208 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 12 | 2 | 28 | 10 | 1 | 2 | 67 | 72 | 98 | 93 |
| Kati | 0 | 0 | 20 | 31 | 93 | 391 | 3 | 13 | 39 | 217 | 107 | 117 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 10 | 11 | 15 | 20 | 51 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 | 26 | 29 | 60 | 19 | 22 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 42 | 31 | 104 | 0 | 29 | 113 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 34 | 39 | 68 | 24 | 24 | 17 |
| Wete | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 12 | 16 | 61 | 92 | 12 | 25 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 11 | 15 | 2 | 0 |
| Chake chake | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 23 | 26 | 14 | 23 | 29 | 19 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 26 | 14 | 13 | 30 | 18 |
| **Zanzibar** | **1** | **0** | **60** | **34** | **166** | **405** | **174** | **191** | **484** | **561** | **465** | **683** |

**Inaendelea… Jadweli 3.6: Takwimu za Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Aprili na Mei 2023**


| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 146 | 55 | 217 | 356 | 0 | 0 | 0 | 642 | 606 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 38 | 268 | 197 | 1 | 0 | 500 | 414 |
| Kati | 27 | 7 | 0 | 0 | 155 | 23 | 335 | 95 | 0 | 0 | 779 | 894 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 80 | 105 | 105 | 94 | 0 | 0 | 227 | 275 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 | 38 | 182 | 103 | 0 | 0 | 269 | 249 |
| Magharibi 'A' | 0 | 34 | 0 | 0 | 99 | 56 | 215 | 186 | 0 | 0 | 489 | 420 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 84 | 133 | 0 | 194 | 206 | 0 | 0 | 453 | 370 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 9 | 28 | 28 | 0 | 0 | 119 | 170 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 | 1 | 9 | 6 | 0 | 0 | 23 | 32 |
| Chake chake | 0 | 2 | 0 | 0 | 10 | 14 | 21 | 12 | 0 | 0 | 98 | 96 |
| Mkoani | 0 | 6 | 0 | 0 | 9 | 18 | 8 | 13 | 0 | 0 | 81 | 94 |
| **Zanzibar** | **27** | **49** | **0** | **238** | **581** | **519** | **1,721** | **940** | **1** | **0** | **3,680** | **3,620** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi, Zanzibar**

**Jadweli 3.7 Tozo zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya kesi, Mei 2023**

| Wilaya | Idadi ya kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 606 | 15,257,000 |
| Kaskazini 'B' | 409 | 7,610,700 |
| Kati | 224 | 10,603,500 |
| Kusini | 204 | 3,220,000 |
| Mjini | 187 | 10,933,600 |
| Magharibi 'A' | 405 | 22,941,950 |
| Magharibi 'B' | 342 | 24,668,000 |
| Wete | 173 | 5,856,500 |
| Micheweni | 32 | 943,000 |
| Chake chake | 72 | 1,510,600 |
| Mkoani | 72 | 1,410,400 |
| **Zanzibar** | **2,726** | **104,955,250** |

**Kielelezo1: Ajali za Barabarani za Barabarani Zilizoripoti kwa Wilaya, Mei 2023**



**Kielelezo 2:Vina na Majeruhi Wanaotokana na Ajali za Barabarani kwa Wilaya, Mei 2023**



**Zingatia Maelezo**

Ajali ya barabarani inahusu ajali yeyote inayohusisha angalau gari moja barabarani, inayotokea barabarani kwa mzunguko wa umma na angalau mtu mmoja amekufa au amejeruhiwa. Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar).

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumia gari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu. Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua, 2321, MMP, Zanzibar
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136